

Wanafunzi wa magari katika Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Veta) wakiwa darasani. **Picha na Maktaba.**

# Serikali yashauriwa kupunguza tozo ya utaalamu nchini

**Waajiri wanasema asilimia 6 ya tozo haifaidishi sekta binafsi na ni asilimia 2 tu ya fedha zinafanya kazi iliyokusudiwa.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kimeitaka Serikali kupunguza tozo ya utaalamu wanayotakiwa kulipa serikalini, kutoka asilimia 6 mpaka 2 kutokana na ukweli kuwa tozo hilo linaongeza gharama za kufanya biashara nchini.

Tozo hilo ambalo lipo kisheria, kwa mujibu wa sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya mwaka 2001 (The Vocational Education and Training Levy Act (2001) inamtaka kila mwajiri, kasoro idara za Serikali, mashirika ya umma, asasi zisizotengeneza faida na zile ambazo zinafanya kazi kwa kupewa fedha na Serikali moja kwa moja, kulipa tozo ya utaalamu ya asilimia 6 kutoka katika jumla ya mishahara ya taasisi husika.

Waajiri wanasema kwamba asilimia hiyo sita ya tozo haifaidishi sekta binafsi na kwamba ni asilimia 2 tu ya fedha zilizochangwa ambazo pia hazifanyi kazi iliyokusudiwa.

"Makusudio ya tozo hayakuwa mabaya, kwa kuwa ililenga kuboresha utaalamu ambao unatakiwa sana katika sekta binafsi, lakini inasikitisha kuona kwamba ni asilimia 2 tu ya fedha hizo zinafanya kazi iliyokusudiwa ya kuwezesha utaalamu," anasema Mkurugenzi wa sera na utetezi wa ATE, Justina Lyela.

Taarifa iliyomo katika ripoti ya utalii iliyokuwa inazungumzia mazingira ya ushindani wa kibiashara ya mwaka 2010 (Competitiveness impacts of Business Environment Reform -CIBER) ambayo inakadiria asilimia 20 hadi 40 ya mafunzo ya ndani katika taasisi mbalimbali yanagusia kutoa utaalamu wa msingi katika shughuli husika (ufundi mchundo).

Ripoti hiyo imesema kwamba wamiliki wa hoteli mathalan, wenye wafanyakazi 135, wanalazimika kuwekeza Sh31.25 milioni kwa mwaka kwa ajili ya utaalamu wa kawaida wa msingi kwa wafanyakazi wao huku wakitakiwa kulipa Sh8 milioni kama tozo ya utaalamu kwa Serikali kila mwaka.

"Uwekezaji ukiwa unafikia asilimia 100 hadi 900 zaidi ya biashara inavyojilipa kwa kuangalia malipo ya tozo la utaalamu (SDL) na asilimia 20 hadi 60 ya mishahara yote," inasema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo kampuni ya utalii yenye wafanyakazi watano na vibarua 10 wahusika wanapaswa kuwekeza Sh5.8 milioni kila mwaka kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi wao huku wakilipa tozo la Sh615,000.

ATE katika taarifa yake inayoelezea msimamo wa kupunguza tozo hilo la utaalamu, wanasema fedha zinazofikishwa Veta hazitoshi japo wao wanakusanya nyingi.

Kutokana na kufikishwa kwa fedha kidogo, Veta inashindwa kutoa wataalamu wengi wenye elimu inayotakiwa katika soko la ajira hivi sasa.

"Hali hiyo siyo tu inazuia waajiri kupata wafanyakazi wenye utaalamu unaotakiwa bila kulazimika kuanza kuwapa mafunzo, lakini inawafanya wafanyakazi wa Tanzania kutokuwa na ushindani unaotakiwa katika soko la ndani na la kimataifa la ajira," inasema ripoti hiyo.



**"Kenya hulipa asilimia moja na si kapuni au mashirika yote yanatakiwa kulipa, tozo hili halipo nchini Rwanda, Uganda na Burundi na kutokana na mazingira hayo unaweza kujiuliza tozo hili linatoa fursa gani ya Tanzania kuhimili ushindani katika soko."**

Justina Lyela

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya msimamo ya ATE, tozo hilo ni sawa na asilimia 4 kwa SDL na kodi nyingine zinazotozwa zinavuruga kabisa mazingira ya kibiashara na kudhoofisha sekta binafsi, hali ambayo imekuwa ikilalamikiwa na waajiri kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa Lyela, tozo la utaalamu ni kubwa kuliko nchi yoyote ile duniani na hata kikanda.

"Kwa mfano Kenya inalia asilimia moja na si kamapuni au mashirika yote yanatakiwa kulipa aidha tozo hili halipo nchini Rwanda, Uganda na Burundi na kutokana na mazingira hayo unaweza kujiuliza tozo hilo linatoa fursa gani ya Tanzania kuhimili ushindani katika soko," anahoji Lyela.

Ingawa Tanzania inaonekana kama mfano mzuri wa kupata fedha kwa ajili ya kutengeneza na kuboresha wataalamu katika elimu ya msingi ya kazi zinazowahusu, asilimia 6 ni kubwa na inafanya kampuni nyingi binafsi kushindwa kuwa katika mfumo thabiti wa uchumi unaoeleweka.

Katika hotuba ya bajeti ya mwaka 2011/12, Serikali ilionyesha kwamba tozo ya SDL itapelekwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB). Mazingira haya mapya na maana ya tozo yenyewe inasababisha kuwapo na haja ya kuangalia upya tozo hilo.

Hata hivyo, ATE inasema kwamba fedha hizo hazistahili kutozwa kwa kuwa wao tayari wanakuwa wamelipa kupitia kodi ya mapato na kodi inayohusu kampuni.

"Tozo la asilimia 4 kwa ajili ya elimu ya juu na tozo la asilimia 2 za stadi za ufundi ina maana kwamba waajiri wanalipishwa kodi mara mbili kwa kuwa ni wajibu wa Serikali kuwekeza katika elimu ya kawaida na chuo kikuu kupitia kodi inazokusanya," inasema ripoti ya ATE.

"Pamoja na gharama yake pia tozo hiyo inatumika visivyo. Fedha hizi zililengwa kupelekwa kwenye ufundi stadi kwa kuwezesha utaalamu ukilinganisha na nadharia zinazopatikana katika elimu ya jumla ikiwamo elimu ya juu," inasema ripoti ya ATE.

Lyela anasema ATE imepeleka taaarifa serikali mara mbili ili ipunguze tozo hilo, lakini hakuna hatua ambayo imechukuliwa.

"Mwaka jana tulipeleka mapendekezo yetu, serikali haikuyapitisha, tumeyapeleka tena mwaka huu tumeambiwa timu maalumu inayoangalia mabadiliko ya kodi Wizara ya Fedha inayafanyia kazi," anasema Lyela

Anabainisha pia kwamba waajiri wengi wanachukua idadi ndogo ya wafanyakazi kwa lengo la kupunguza gharama inayotokana na tozo hilo na matokeo yake ni kuongezeka kwa watu wasiokuwa na kazi.

Kwa mujibu wa taarifa ya ATE, shughuli ya kukusanya tozo hilo haziridhishi kutokana na ukweli kwamba si kila mwajiri katika sekta binafsi analipa. Wengi hawalipi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kodi kubwa. Kwa mujibu wa taarifa hiyo kodi hiyo kubwa, inasababisha kamapuni nyingi za watu binafsi kufanya kazi bila kusajiliwa kama njia ya kuikwepa kodi hiyo.

"Matokeo yake ni biashara chache zilizosajiliwa zinakuwa na mzigo wa kulipia tozo hilo nchini wakati kampuni nyingine nyingi zikifaidi utaalamu unaowezeshwa na SDL.

**Tujadliane kupitia Ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatiwa na ujumbe. Ujumbe wako mfupi ni bure, hautozwi.**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI